**MKOA WA NJOMBE**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**

***(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)***

**Barua pepe: ded.wangingombe@njombe.go.tz**
**Simu: 0765024668**
**MKURUGENZI MTENDAJI**

**KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI**
**WILAYA YA WANGING'OMBE**
**S.L.P. 64**
**NJOMBE.**

**02/10/2017**

# TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI

## KIPINDI CHA KUANZIA JULAI HADI SEPTEMBA 2017

## UTANGULIZI

Taarifa hii ya Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2017 imezingatia Sheria na Miongozo ya matumizi ya fedha za Serikali ambazo ni Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013, Sheria ya fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, Muongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta za Umma wa mwaka 2015, Muongozo wa Uhasibu wa mwaka 2010 na Muongozo wa fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009.

## MAJIBU YA HOJA ZA NYUMA ZA MKAGUZI WA NDANI

| NA. | HOJA | MAJIBU YA MENEJIMENTI | MAONI YA MKAGUZI |
|---|---|---|---|
| 1 | Malipo yanayotia mashaka Tsh 4,434,455 | - Ushauri wa mkaguzi umezingatiwa.<br>Barua yenye kumb.no.CIC/F/2 ya tarehe 10/2/2017 ya kukumbushia madai haya imeambatanishwa. Tazama kiambata no.1, Mtumishi atanza kukatwa mshahara kuanzia mwezi April 2017 ili kufidia kiasi tajwa cha Tsh 2,500,000 ambacho anadaiwa kama masurufu. | Hoja haijafungwa.<br>Utekelezaji wake bado haujaanza kufanyika. |
| 2 | Mikopo iliyokopeshwa kwa vikundi vya Vijana na Wanawake ambayo haijarejeshwa Tsh 11,795,000 | Menejimenti imezingatia ushauri wa Mkaguzi.<br>Ufuatiliaji umeendelea kufanyika kuhakikisha mikopo hiyo inarejeshwa na baadhi ya vikundi vimerejesha Jumla ya Tsh 2,804,250 na kubaki kiasi cha Tsh 3,945,750 ambacho ufuatiliaji unaendelea kufanyika. | Hoja haijafungwa.Itafungwa utekezaji wake ukikamilika.<br>Mikopo ilibaki kurejeshwa ni Tsh 1,780,000.00 mfuko wa Wanawake na Tsh 2,165,750 mfuko wa vijana ambayo jumla yake ni Tsh 3,945,750. |
| 4 | Malipo yaliyofanyika nje ya bajeti Tsh 2,920,000 | Menejimenti imezingatia ushauri wa Mkaguziwa Ndani. Marekebisho ya bajeti yalifanyika wakati wa kuanza mfumo wa epicor. | Hoja imefungwa. |
| 5 | Watumishi kutopewa stahili zao | Ushauri wa mkaguzi umezingatiwa.Mtumishi tajwa atalipwa stahiki zake zilizobaki na vielelzo kuwasilishwa kwa Mkaguzi wa Ndani kwa ajili ya uhakiki | Hoja haijafungwa.Utekelezaji wake bado haujafanyika |
| 6 | Manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya masurufu (Micro Procurements) Tsh 440,000 | Ushauri wa mkaguzi umezingatiwa.Manunuzi haya yalifanyika wakati wahusika waufungaji wa hesabu wakiwa nje ya ofisi kikazi (makambako).<br>Hata hivyo taarifa hiyo imeandaliwa na kuwasilishwa kwa uhakiki. | Hoja imefungwa.<br>Utekelezaji wake umefanyika. |
| 7 | Taarifa ya Manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya masurufu (Micro Procurements) | Ushauri umezingatiwa. | Hoja imefungwa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kutoandaliwa Tsh 5,376,600. | Hata hivyo taarifa hiyo imeandaliwa na kuwasilishwa kwa uhakiki. | Utekelezaji wake umefanyika. |
| 8 | Malipo yaliyolipwa kuzidi kiwango stahili Tsh 160,000 | Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa.<br><br>Marekebisho yamefanyika kwani kulikua na makosa ya uchapaji. Marekebisho hayo yamewasilishwa kwa ajili ya uhakiki. | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki umefanyika |
| 9 | FEDHA ZA MIRADI YA MAJI (RWSSP)<br><br>i. Malipo yenye nyaraka pungufu Tsh 167,805,393.30 | Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa.<br>Viambatanisho vimewasilishwa kwa ajili ya uhakiki.<br>Hata hivyo kwa malipo ya Tsh 158,266,481 aliyolipwa Mkandarasi kwa kazi ya uchimbaji visima Halmashauri imeandika barua yenye kumbu.LGA/153/2016/2017/W/09/06 ya tarehe 03/05/2017 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuomba msamaha wa kodi ili mkandarasi aweze kutoa stakabadhi ya kielekroniki kwasababu miradi hii ina msamaha wa kodi. | Hoja haijafungwa.<br><br>Viambatanisho vya Tsh 158,266,481 havijawasilishwa kwa ajili ya uhakiki. |
| | **FEDHA ZA MFUKO WA PAMOJA WA AFYA (HEALTH BUSKET FUND) KATIKA HOSPITALI YA ILEMBULA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 NA 2016/2017**. | | |
| 10 | Malipo yaliyofanyika nje ya bajeti Tsh 1,380,000 | Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa.<br>Maelekezo yameshatolewa kwa Watumishi wa Ilembula wanaohusika na masuala ya fedha juu ya masuala ya kiuhasibu na manunuzi. | Hoja imefungwa. |
| 11 | Malipo yaliyofanyika kabla ya mapokezi ya dawa na vifaa tiba Tsh 11,913,050 | Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa.<br><br>Maelekezo yameshatolewa kwa Watumishi wa Ilembula wanaohusika na masuala ya fedha juu ya masuala ya kiuhasibu na manunuzi. | Hoja imefungwa. |
| 12 | Manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya masurufu (Micro Procurements) kutokua na vithibisho Tsh 130,000. | Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa.<br><br>Stakabadhi ya Tsh 100,000 imeambatanishwa kwa uhakiki wa mkaguzi. | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki umefanyika. |
| 13 | Halmashauri kutaonza | Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa. | Hoja haijafungwa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kutekeleza sera ya vihatarishi | Halmashauri bado ipo katika maandalizi ya awali ya kuandaa leja za vihatarishi. | Utekelezaji wake haujaanza. |
| 14 | Jamii kutochangia miradi ya maendeleo | Ushauri umezingatiwa.<br><br>Menejimenti itaendelea na juhudi za kufanya uhamasishaji ili jamaa iweze kuchangia michango hiyo. | Hoja imefungwa.<br><br>Menejimenti inasisitizwa kuendelea kufanya uhamasishaji ili jamii ione umuhimu wa kuchangia miradi ya maendeleo na kutimiza kwa wakati malengo yaliyowekwa. |
| 15 | Manunuzi yaliyofanyika nje ya bajeti na mpango wa manunuzi Tsh 68,538,350.41 | Ushauri umezingatiwa.<br><br>Marekebisho ya vifungu hivyo yameshafanyika kwenye wakati wa kuingiza matumizi yote ya mwaka katika mfumo | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki umefanyika |
| 16 | Madeni ya wazabuni ya muda mrefu ambayo hayajalipwa Tsh 10,584,982.00 | Ushauri umezingatiwa.<br><br>Mernejimenti inalifanyia kazi kwa kupunguza madeni hayo kadiri fedha zinapopatikana .kwa sasa kiasicha Tshs 5,500,000.00 kimetegwa kupunguza madeni ya nyuma na vielelezo vimewasilishwa kwa Mkaguzi kwa uhakiki. | Hoja imefungwa.<br><br>Ufuatiliaji utaendelea kufanyika katika kaguzi zinazofuata. |
| 17 | Mikataba ambayo haijaingizwa kwenye leja ya mikataba Tsh 3,549,762,589.53 | Ushauri umezingatiwa.<br><br>Mikataba hiyo imeshaingizwa kwenye leja na leja imeawasilishwa kwa Mkaguzi kwa uhakiki | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki umefanyika. |
| 18 | Masurufu ambayo hayajarejeshwa Tsh 3,999,500 | Ushauri umezingatiwa.<br><br>Masurufu hayo yamesharejeshwa na leja ya masurufu imewasilishwa | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki umefanyika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kwa ajili ya uhakiki. | |

**HOJA ZA MKAGUZI WA NDANI ZA ROBO YA NNE KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI HADI SEPTEMBA 2017.**

| NA. | HOJA | MAJIBU YA MENEJIMENTI | MAONI YA MKAGUZI |
|---|---|---|---|
| i | **Malipo yaliyofanyika bila ya kupitia ukaguzi wa awali (pre-audit) Tsh 7,450,500**<br><br>**Hali ilivyo** | Mapungufu yaliyojitokeza yamefanyiwa kazi kwa | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Ukaguzi umebaini kuwapo kwa malipo ya jumla ya Tsh 7,450,500 yaliyofanyika bila ya kufanyiwa ukaguzi wa awali (pre-audit) hali inayoweza kupelekea kufanyika kwa urahisi ubadhilifu wa fedha. Hii ni kinyume na taratibu za malipo ya fedha za Serikali. **Angalia kiambatanisho A.**<br><br>Ukaguzi wa awali husaidia kuhakiki uhalali wa nyaraka na malipo husika kwani mhusika wa kitengo hiki hugonga mhuri, huandika saini na tarehe ya ukaguzi huo wa awali baada ya kujiridhisha na uhalali wa malipo husika.<br><br>**Sheria iliyovunjwa**<br>- Muongozo wa Uhasibu wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2010 (Local Authority Accounting Mannual 2010) kifungu cha 2.4.2 kinachohusu uandishi na uidhinishaji wa hati za malipo na kinachoeleza hati za malipo na nyaraka zingine halisi kupita kitengo cha ukaguzi wa awali kabla ya malipo kufanyika ili kuhakiki usahihi na uhalali wake.<br><br>**Sababu za hali hii**<br>- Kutozingatia miongozo ya matumizi ya fedha za Serikali.<br><br>**Athari za hali hii**<br>- Halmashauri kupata hoja za kiukaguzi.<br>- Malipo kufanyika zaidi ya mara moja kwa kutumia nyaraka moja hali inayoweza kusababisha ubadhilifu au matumizi mabaya ya fedha za Serikali kutokea ambayo yataathiri malengo yaliyowekwai.<br><br>**Ushauri**<br>- Menejimenti ihakikishe malipo yote yanafanyiwa ukaguzi wa awali kabla ya malipo kufanyika ili kuzuia upotevu/ubadhilifu wa fedha za Serikali tajwa hapo juu. | kupitia malipo yote yaliyokuwa hayajakaguliwa. Hati zote za malipo zimewasilishwa kwa uhakiki | umefanyika |
| **ii** | **Malipo yaliyofanyika bila kufuata taratibu za malipo Tsh 7,245,000**<br>**Hali ilivyo**<br>Ukaguzi umebaini kuwapo kwa malipo ya jumla ya Tsh 7,245,000 yaliyofanyika bila kufuata taratibu | Malipo yaliyofanyika bila kufuata taratibu za malipo ya Tsh 7,245,000 | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | za malipo kama mapungufu hayo yanavyoonekana katika **kiambatanisho B.**<br><br>**Sheria iliyovunjwa**<br>- Muongozo wa Uhasibu wa Serikali za Mitaa 2010 (LAAM ,2010)), vifungu vya 2.4.1 na 2.4.2 na Muongozo wa fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009, kifungu cha 11 (2) (a) na (c) na kifungu cha 71 (f) vinavyoagiza kuwapo kwa idhini za malipo na uandishi sahihi wa nyaraka zote za malipo kabla ya malipo kufanyika.<br><br>**Sababu za hali hii**<br>- Uhaba wa Watumishi katika Idara ya Fedha.<br><br>**Athari za hali hii**<br>- Halmashauri kupata hoja za kiukaguzi.<br>- Ubadhilifu wa fedha za Serikali ambayo yanaweza kusababisha malengo yaliyowekwa kutofikiwa au kufikiwa kwa kiwango cha chini.<br><br>**Ushauri**<br>- Mapungufu hayo yarekebishwe na vielelezo kuwasilishwa Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani kwa ajili ya uhakiki.<br>- Halmashauri ifanye jitihada za kuwasiliana na Mamlaka za uajiri ili kuongeza Watumishi Idara ya Fedha kwa lengol la kuongeza ufanisi wa kazi ili kuepuka athari tajwa hapo juu. | yamefanyiwa kazi kwa kuidhinisha fomu ambazo zilikuwa hazijakamilika na vielelezo hiyo vimewasilishwa kwa uhakiki. | umefanyika |
| **iii** | **Taarifa ya Manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya masurufu (Micro Procurements) kutowasilishwa kwenye Bodi ya zabuni na Mamlaka Tsh 1,750,000**<br><br>**Hali ilivyo**<br>Ukaguzi umebaini kutokuwapo kwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Bodi ya Zabuni na Mamlaka husika ya manunuzi ya jumla ya Tsh 1,750,000 yaliyofanyika kwa njia ya masurufu (Micro Procurements) kama Kanuni za Manunuzi ya Umma zinavyoagiza. **Angalia kiambatanisho C.**<br><br>Kwa mujibu wa Kanuni za Manunuzi ya Umma mwaka 2013, Manunuzi yote yanayofanywa kwa njia | Ushauri umezingatiwa.<br><br>Taarifa itaandaliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki. | Hoja haijafungwa.<br><br>Utekelezaji wake haujafanyika. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ya masurufu (Micro Procurements) taarifa yake hupaswa kuwasilishwa kila mwezi katika Bodi ya Zabuni na kila robo kwa Mamlaka husika.<br><br>**Sheria iliyovunjwa**<br><br>- Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 kifungu cha 166 (7) na (8) kinachoagiza taarifa za manunuzi kwa njia ya masurufu kuwasilishwa kila mwezi katika Bodi ya Zabuni na kila robo kwa Mamlaka.<br><br>**Sababu za hali hii**<br>- Kutofuata Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma.<br><br>**Athari za hali**<br>- Halmashauri kupata hoja za kiukaguzi.<br><br>**Ushauri**<br>- Taarifa hizo ziandaliwe na kuwasilishwa kwenye Bodi ya Zabuni na Mamlaka husika kama Kanuni za Manunuzi ya Umma zinavyoagiza. | | |
| **iv** | **Malipo ya manunuzi kinyume na taratibu Tsh 1,888,150**<br><br>**Hali ilivyo**<br>Ukaguzi umebaini kuwapo kwa manunuzi ya jumla ya Tsh 1,888,150 yaliyolipwa bila huduma kupokelewa kama Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma zinavyoagiza malipo kufanyika baada ya huduma kupokelewa. Hii ni kutokana na kutokuwapo kwa Hati za mapokezi ya stoo (Delivery Notes) ambazo ndio vithibitisho vya kupokea huduma husika. **Angalia kiambatanisho D**.<br>**Sheria iliyovunjwa**<br><br>- Muongozo wa fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 kifungu cha 22 (2) kinachoagiza malipo kutofanyika mpaka huduma husika iwe imepokelewa.<br><br>**Sababu za hali hii** | Hati za mapokezi ya stoo (Delivery Notes) zenye jumla ya Tshs 1,888,150.00 zimeambatanishwa na kuwasilisha kwa mkaguzi kwa uhakiki. Malipo haya ni yale ya mradi wa boresha afya ambapo baada ya malipo nakala halisi (Original document) hutumwa | Hoja imefungwa.<br><br>Uhakiki umefanyika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | - Kutozingatiwa kwa sheria na miongozo ya matumizi ya fedha za Serikali<br><br>**Athari za hali hii**<br><br>- Halmashauri kupata hoja za kiukaguzi zinazoweza kuisababishia Halmashauri kupata hati zisizoridhisha.<br>- Matumizi mabaya ya fedha za Serikali ambayo yanaweza kusababisha malengo yaliyowekwa kutofikiwa au kufikiwa kwa kiwango cha chini.<br><br>**Ushauri**<br><br>- Sheria na Miongozo ya fedha za Serikali ifuatwe ili kuepuka athari tajwa hapo juu. | kwao. | |
| v | **Malipo yenye nyaraka pungufu Tsh 470,922,814.00**<br><br>**Hali ilivyo**<br><br>Ukaguzi umebaini kuwapo kwa malipo ya jumla ya Tsh 470,922,814.yenye nyaraka pungufu kutokana na matumizi mbalimbali ya fedha yaliyofanyika katika kipindi husika.<br><br>Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika **kiambatanisho E.**<br><br>**Sheria iliyovunjwa**<br><br>- Muongozo wa fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 kifungu cha 8 (2) (c) na kifungu cha 10 (2) (d) vinavyoagiza matumizi yoyote ya fedha ya Serikali kuwa na kithibitisho cha uhalali wa matumizi hayo ambacho kinapaswa kuambatanishwa katika nyaraka ya malipo husika.<br><br>**Sababu za hali hii**<br><br>- Kutozingatiwa kwa sheria na miongozo ya fedha iliyowekwa. | Hoja hii inafanyiwa kazi na vielelezo vikikamilika vitawasilishwa kwa Mkaguzi kuhakikiwa. | Hoja haijafungwa.<br><br>Utekelezaji bado haujafanyika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | - Uhaba wa Watumishi katika Idara ya Fedha kwa ajili kufanya ufuatiliaji wa nyaraka na utunzaji wa kumbukumbu.<br>**Athari za hali hii**<br>- Halmashauri kupata hoja za kiukaguzi.<br>**Ushauri**<br>Viambatanisho vilivyokosekana viambatanishwe na kuletwa Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani kwa ajili ya uhakiki. | | |

**Changamoto**

- Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani ina mtumishi mmoja na hivyo kuathiri shughuli za ukaguzi.
- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kutokua na usafiri na hivyo kuathiri shughuli za Mkaguzi wa Ndani.
- Bajeti finyu ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani toka Serikali kuu na Mapato ya Ndani iliyotengwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya shughuli za Mkaguzi wa Ndani.

Angumbwike S. Paul
**Mkaguzi wa Ndani**
**Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe**

**KIAMBATANISHO A**

| TAREHE | NA.HATI YA MALIPO | NA.HUNDI | KIASI KILICHOLIPWA TSH | MLIPWAJI | AKAUNTI YA MALIPO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 24/08/2017 | 9/8 | 000860 | 600,000 | RIANA COMPUTER | Amana | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa shajala. |
| 24/08/2017 | 10/8 | 000861 | 1,000,000 | RIANA COMPUTER | Amana | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa shajala. |
| 21/09/2017 | 6/9 | 000218 | 3,430,000 | Mwakindole Food Catering and decoration | Amana | Malipo ya huduma ya chakula |
| 21/09/2017 | 7/9 | 000219 | 300,000 | Nivahe Stephen | Amana | Malipo ya posho kwa kazi ya usaili wa Wanafunzi wa darasa la saba |
| 26/09/2017 | 41/9 | 004590 | 2,120,500 | NMB PLC | Amana | Malipo ya posho ya Wajumbe wa kamati ya kuhakiki mali za NJODECO |
| | | **Jumla kuu** | **7,450,500** | | | |

**KIAMBATANISHO B**

| TAREHE | NA.HATI YA MALIPO | NA.HUNDI | KIASI KILICHOLIPWA TSH | MLIPWAJI | AKAUNTI YA MALIPO | MAELEZO | MAPUNGUFU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 07/09/2017 | 5/9 | 004554 | 1,560,000 | CASH | Matumizi Mengineyo | Malipo ya posho ya Viongozi wa Halmashauri kushiriki ufunguzi na kilele cha Maonesho ya Nane Nane | Fomu za safari hazijaidhinishwa na Mkuu wa Idara na Mwekahazina |
| 16/09/2017 | 4/9 | 002467 | 1,080,000 | NMB PLC | Maendeleo (UNICEF) | Malipo ya posho ya kujikimu kwa timu ya ukaguzi wa miradi | Fomu za safari hazijaidhinishwa na Mkuu wa Idara na Mwekahazina |
| 27/09/2017 | 61/9 | 004605 | 1,750,000 | Yusufu Ahmadi | Matumizi mengineyo | Masurufu kwa ajili ya ununuzi wa chakula kwa matumizi na uingizaji Taarifa za FFARS | Fomu ya masurufu haijaidhinishwa na Mwekahazina |
| 27/09/2017 | 56/9 | 004599 | 1,330,000 | CASH | Matumizi Mengineyo | Gharama ya kuendesha kikao cha Kamati ya | Fomu ya maombi ya fedha |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Ukaguzi | haijaidhinishwa na Afisa Masuuli |
| 28/09/2017 | 7/9 | 000868 | 1,525,000 | CASH | Amana | Malipo ya posho kwa wajumbe waliofanya kazi ya ufuatiliaji mradi wa ujenzi wa P4R katika shule ya Sekondari Kipengere | -Fomu za safari hazijaidhinishwa na Mwekahazina.<br>- Hakuna vifungu vya malipo kwenye fomu za safari |
| | | **Jumla kuu** | **7,245,000** | | | | |

**KIAMBATANISHO C**

| TAREHE | .HATI YA MALIPO | HUNDI | KIASI TSH | MLIPWAJI | AKAUNTI YA MALIPO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 27/09/2017 | 61/9 | 004605 | 1,750,000 | Yusufu Ahmadi | Matumizi mengineyo | Masurufu kwa ajili ya ununuzi wa chakula kwa matumizi na uingizaji Taarifa za FFARS |
| | | **Jumla kuu** | **1,750,000** | | | |

**KIAMBATANISHO D**

| TAREHE | NA.HATI YA MALIPO | NA.HUNDI | KIASI KILICHOLIPWATSH | MLIPWAJI | AKAUNTI YA MALIPO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 24/08/2017 | 9/8 | 000860 | 600,000 | RIANA COMPUTER | Amana | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa shajala. |
| 24/08/2017 | 10/8 | 000861 | 1,000,000 | RIANA COMPUTER | Amana | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa shajala. |
| 28/09/2017 | 13/9 | 000874 | 288,150 | TEMESA-NJOMBE | Amana | Gharama za Matengenezo ya gari DFPA 2112 |
| | | **Jumla kuu** | **1,888,150** | | | |

**KIAMBATANISHO E**

| **TAREHE** | **NA.HATI YA MALIPO** | **NA.HUNDI** | **KIASI KILICHOLIPWA TSH** | **MLIPWAJI** | **AKAUNTI YA MALIPO** | **MAELEZO** | **KIAMBATANISHO KINACHOKOSEKANA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 25/08/2017 | 1/8 | 000735 | 312,734,467.80 | NMB PLC | NWSDP | Malipo kwa ajili ya usambazaji wa mabomba ya maji kwa kampuni ya PIPE INDUSTRY CO.LTD | Stakabadhi ya Kielektroniki |
| 25/08/2017 | 2/8 | 000735 | 130,883,346.20 | NMB PLC | NWSDP | Malipo kwa ajili ya ujenzi wa kisima cha maji katika kijiji cha Isindagosi kwa kampuni ya SEBA CONSTRUCTION LTD | Stakabadhi ya Kielektroniki |
| 16/09/2017 | 4/9 | 002467 | 1,080,000 | NMB PLC | Maendeleo (UNICEF) | Malipo ya posho ya kujikimu kwa timu ya ukaguzi wa miradi | -Orodha ya Walipwaji.<br>-Taarifa ya kazi |
| 11/09/2017 | 3/9 | 000215 | 450,000 | NMB PLC | Elimu | Malipo ya posho ya masaa ya ziada kwa shughuli za | Orodha ya Walipwaji |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | ufuatiliaji wa magari, mafuta na ujazaji wa vitabu vya safari na kuandaa mikataba | |
| 21/09/2017 | 6/9 | 000218 | 3,430,000 | Mwakindole Food Catering and Decoration | Amana | Gharama ya huduma ya chakula kwa ajili ya wajumbe walioshiriki semina ya kazi maalum | Fomu za mahudhurio |
| 22/09/2017 | 5/9 | 002468 | 19,820,000 | CASH | Maendeleo (UNICEF) | Malipo ya posho kwa washiriki wa mafunzo ya TUSEME na GRP. | Fomu za mahudhurio |
| 27/09/2017 | 48/9 | 004597 | 1,000,000 | NMB PLC | Matumizi Mengineyo | Punguzo la deni la mchango wa ALAT | Stakabadhi |
| 28/09/2017 | 7/9 | 000868 | 1,525,000 | CASH | Amana | Malipo ya posho kwa wajumbe waliofanya kazi ya ufuatiliaji mradi wa ujenzi wa P4R katika shule ya Sekondari Kipengere | Taarifa ya Kazi |
| | | **Jumla kuu** | **470,922,814.00** | | | | |